**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2**
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2**

Tuesday 11 May 2004 (morning)
Mardi 11 mai 2004 (matin)
Martes 11 de mayo de 2004 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works, will not score high marks.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3e partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2e partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3e partie n'obtiendront pas une note élevée.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Andika insha kujibu moja ya masuala yafwatayo. Jibu lako lazima liwe juu ya angalau kazi mbili za sehemu ya 3 ulizojitayarisha nazo. Lazima uingize katika jibu lako mjadala wa kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu huohuo mmoja kama inavyohusika. Majibu ambayo hayaegemei mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapata alama za juu.*

**Tamthilia**

**1.** *Ama*

(a) Kwa kutumia tamthilia mbili ulizozisoma katika sehemu hii, onyesha vipi *sauti* na *kicheko* hutumiwa katika tamthilia hizo kuimarisha fani na maudhui.

*Au*

(b) Kwa kutumia tamthilia mbili ulizozisoma linganisha 'migogoro' mbalimbali inavyojitokeza.

**Riwaya**

**2.** *Ama*

(a) Linganisha riwaya mbili ulizozisoma katika sehemu hii, ukionyesha jinsi zinavyotumia mbinu ya usimulizi.

Au

(b) "Lugha ni kipengele muhimu kinachotofautisha waandishi wawili kimtindo." Huku ukitoa mifano kutoka riwaya mbili ulizozisoma, onyesha mitindo ya waandishi wake inavyotofautiana kilugha.

**Ushairi**

**3.** *Ama*

(a) Kwa kutumia baadhi ya mashairi kutoka diwani mbili za mashairi ulizozisoma, jadili nakuonyesha umuhimu wa ujenzi wa picha katika mashairi hayo.

*Au*

(b) "Kaida – yaani matumizi ya beti, vina na mizani ni kanuni za mshikizo na kupita tu."Je, unakubaliana na kauli hii? Ijadili kwa kuitolea mifano kutokana na baadhi ya mashairi ya diwani mbili ulizozisoma.

**Riwaya ya Mapenzi**

**4.** *Ama*

(a) Katika riwaya mbili ulizozisoma katika sehemu hii onyesha kama wahusika wa kiume wanachorwa kwa upendeleo zaidi kuliko wahusika wa kike.

*Au*

(b) "Mapenzi maana yake kuyarutubisha au kuyavunja makubaliano yake." Ijadili kauli hii kwa kutoa mifano kutoka angalau kazi mbili ulizozisoma katika sehemu hii.

**Masuala ya Ujumla**

**5.** *Ama*

(a) "Waandishi wa tamthilia, tofauti na wa riwaya, hawana nafasi ya kusimulia kila kitu, kwa sababu katika tamthilia vitendo na udhahiri wa mambo hutawala zaidi." Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutokana na angalu tamthilia na riwaya moja uliyosoma.

*Au*

(b) "Fasihi huathiriwa sana na matokeo muhimu yanayozuka katika jamii fulani – yawe ya kihistoria, kidini, kisiasa au kijamii." Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano mbalimbali ya kazi mbili ulizozisoma.

*Au*

(c) "Mpangilio wa sauti katika kujenga muziki ni kipengele muhimu sana katika ushairi wowote ule." Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutokana na kazi mbili za ushairi ulizozisoma.

*Au*

(d) "Mwandishi na anachokiandika ni zao la jamii." Kutokana angalau kazi mbili ulizozisoma, onyesha jinsi waandishi na kazi zao zinavyoathiriwa na jamii walimokulia.